# Vitangishi na Utata katika Tungo za Kiswahili: Uchambuzi wa Kinadharia

*Joash J. Gambarage*

**Ikisiri**

*Vitangishi vinatajwa kuwa na mchango mkubwa katika kuyaeleza mahusiano ya kitanzu katika lugha nyingi, kama siyo zote, ulimwenguni. Stadi za vitangishi zinaripoti kujumuisha viwango mbalimbali vya lugha kama vile: mofolojia, sintaksia, semantiki, na pragmatiki. Vitangishi vinafahamika kwa tabia yake ya kuleta utata katika tungo pale ambapo hutokea katika tungo na kirai kitangishi kingine, kirai nomino (KN), kirai kibainishi au kiashiria kingine cha kimantiki kama vile ukanushi au kiulizi (taz. Matthewson, 1998; Krifka, 2003). Kutokana na tabia hii, vitangishi hufasiliwa kwa kuhusisha viwango vya lugha zaidi ya kimoja. Kadhalika, stadi za vitangishi katika 'nadharia rasmi' za isimu zimegubikwa na matumizi ya alama za kimantiki* $\forall$, $\exists$, *na nyinginezo; alama ambazo zimekithiri matumizi yake katika sematiki ya vitangishi na vibainishi tangu kazi za awali za kimantiki za Pierce (1870), Frege (1892) na Russell (1905). Makala haya yatajadili vitangishi viwili tu: vitangishi-ulimwengu na vitangishi-kuna, na kuonesha jinsi matumizi ya virai vitangishi hivi yanavyoleta utata katika tungo za Kiswahili. Lengo la makala haya ni kuibua vionjo juu ya kaida za vitangishi, mbinu za kubaini na kukabiliana na utata wa tungo unaojitokeza kutokana na matumizi ya vitangishi katika lugha ya Kiswahili.*

## 1.0 Utangulizi

Vitangishi ni aina ya maneno ambayo huifanya nomino iliyokumbwa na kitangishi kufasilika kulingana na 'mawanda ya kisarufi' iliyoyachukua dhidi ya kirai-kitangishi kingine au viashiria vingine vya kimantiki[1] (taz. Kratzer, 1998; Matthewson, 1999). Kwa fasili hii, nomino inaweza kuchukua 'mawanda-pana', 'mawanda-kati' au 'mawanda-finyu' dhidi ya viashiria vingine vya kimantiki au nomino zilizotumika na viashiria hivyo. Hivyo basi, vitangishi huingiliana kimawanda na vitangishi vingine au viashiria vya kimantiki katika tungo. Katika hali hii, tungo huzongwa na utata ambao huweza kufasilika kwa kanuni za uhamishaji virai vitangishi za kisintaksia. Hivyo, KN hutangishwa kimaana pale inapokumbwa na kitangishi husika kilichojikita katika mawanda yake. Tuangalie

[1] Katika makala haya nimetumia dhana ambazo zinaweza kuwa na matumizi tofauti katika nyanja fulani. Kwa mfano, neno mawanda lilivyotumika hapa siyo sawa na litumikavyo katika njanja za fasihi. Nimetumia dhana zilizopo katika Kiswahili kuelezea lugha ya kiufundi ambayo hutumika katika taaluma zinazojadiliwa hapa. Dhana ya utangishaji 'quantification' si ubunifu wa mwandishi. Dhana hii imetumika katika matini ya semantiki ya Profesa Kulikoyela Kahigi aliyekuwa mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Nimeona dhana hii inafaa kuliko ile ya viidadi. Orodha ya msamiati imewekwa mwisho.

mfano (1) kutoka katika lugha ya Kiingereza unaonesha kubadilishana mawanda kwa vitangishi-jumui kama vile *most* '-ingi', *every* 'kila', na *some* 'fulani' uliotolewa na Matthewson (1999: 84).

(1) Most linguists have looked at every analysis that solves some problem.

Matthewson akitumia nadharia ya kisemantiki ya *Choice Function* ya Reinhart (1997) pia Winter (1997), ambayo hatutaweza kutoa maelezo yake ya kina hapa, anatoa fasili tatu za mfano uliotolewa katika (1) juu kama ifuatavyo [Msisitizo ni wangu].

(i) 'There is *some problem*, such that *most linguists* have looked at every analysis that solves that problem.'

(ii) 'For *most linguists*, there is *some problem*, such that they have looked at *every analysis* that solves that problem.'

(iii) '*Most linguists* have looked at *every analysis* that solves *a problem*.'

Tafsiri ya kitangishi *some* katika Kiswahili tutaijadili katika sehemu ya 3.1.2 ya makala haya. Msomaji anaweza kuona wazi kuwa kitangishi *some* kimechukua mawanda-pana katika (i) kwa kutokea kabla ya vitangishi vingine katika sentensi. Kwa maana iliyotolewa katika (ii), kitangishi hichohicho kinachukua mawanda-kati kwa kutokea katikati ya virai vitangishi vingine. Maana ya tatu inayotolewa na Matthewson inajichomoza baada ya kirai-kitangishi kilekile kutokea mwishoni mwa sentensi, yaani kimechukua mawanda-finyu kwa kutokea baada ya virai vitangishi vyote. Uhamishaji huu ni maarufu kwa jina la uhamishaji wa virai vitangishi (tàz. Reinhart, 1997; Kratzer, 1998; Carnie, 2007 na wengine kwa dhana ya 'upelekaji mbele wa vitangishi'). Hata hivyo, si wakati wote uhamishaji wa virai vitangishi unakuwa wa kuonekana/wa wazi. Wakati mwingine unakuwa wa mficho, tutauita "uhamishaji-fiche" utokeao katika akili ya msemaji (umbo mantiki la lugha) lakini haujidhihirishi katika 'umbo fonetiki la lugha' (taz. Chomsky, 1995, 2000, 2001). Huu ni mwanzo wa kuthibitisha dai kwamba hatuwezi kujadili dhana za vitangishi bila kuhusisha viwango vingine vya lugha.

Makala haya yana sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza ni utangulizi. Sehemu ya pili inazungumzia kwa kifupi taipolojia ya vitangishi na kueleza kwa kirefu aina za vitangishi katika Kiswahili na mahusiano yake kimawanda katika tungo. Sehemu ya tatu inajadili mbinu rasmi/za kinadharia zinazopendekezwa katika kupanga mawanda na kuyafasili. Sehemu ya nne ni hitimisho.

## 2.0 Vitangishi: Kiswahili na Lugha nyingine

Lugha ya Kiswahili imebahatika kuwa na vitangishi kadhaa ambavyo hutofautiana kimaana na kimatumizi katika tungo. Hata hivyo, kitaipolojia, lugha moja inaweza kuwa na vitangishi vingi kuliko lugha nyingine. Lugha nyingi za Kibantu, kwa mfano, huwa na tabia ya kulundika pamoja 'fahiwa' za baadhi ya vitangishi ambavyo katika lugha nyingine huwa ni fahiwa tofauti. Kwa mfano, katika

Kiswahili kitangishi *kila* hutafsirika kwa Kiingereza kama '*every*' au '*each*'. Katika Kiingereza vitangishi '*every*' na '*each*' hutofautiana kidhima japo kwa namna moja au nyingine ni fahiwa zinazoshabihiana (rej. Begheli na Stowell, 1996; Kratzer na Heim, 2010 kwa mjadala). Lugha nyingine za Kibantu hutumia leksimu moja kwa fahiwa mbili tofauti kabisa. Mfano wa lugha hizo ni Kinata kinachozungumzwa mkoani Mara, Tanzania. Kwa maelezo ya Gambarage (2012) kitangishi '-ote' na kitangishi 'kila' katika lugha hii hutafsirika kama '*-ose*'. Kinachosaidia kujua kama Mnata amesema 'watoto wote' au 'kila mtoto' ni mofolojia ya Kinata ambapo '*-ose*' ikitumika na nomino ya umoja humaanisha kitangishi 'kila'; lakini kitangishi hichohicho kikitumika na nomino ya wingi humaanisha '-ote'. Hali hii imewafanya Wanata kuazima kitangishi 'kila' katika Kiswahili na kukitumia mahali pa -ose ya umoja.

**2.1 Aina za Vitangishi katika Kiswahili na Mbinu ya Kufasili**

Kabla ya kutaja aina za vitangishi ni muhimu kueleza kuwa hakuna uainishaji unaoweza kutosheleza madai yote ya kinadharia. Uainishaji wangu utaegemea katika mahusiano ya kimofosintaksia na kisintaksia-semantiki/pragmatiki. Aidha, fasili ya mawanda ya virai vitangishi hutegemeana na vipashio vinavyohusiana na vitengo tajwa. Uainishaji huu unashabihiana na ule wa Szabolcsi (1996) pia Begheli na Stowell (1996). Baadhi ya vitangishi katika Kiswahili ni kama vile:

(i) Vitangishi-ulimwengu: kwa mfano *kila* na *-ote*.
(ii) Vitangishi-kuna: kwa mfano *fulani, baadhi, kadhaa, chache, -ingi,* n.k.

Aina nyingine za vitangishi ni kama vile:

(iii) Vitangishi namba: kwa mfano *moja, tano, saba* n.k.
(iv) Vitangishi masharti vyenye mpaka wa kiasi au idadi ya kuanzia na/au ya kuishia: kwa mfano: *pungufu ya tatu, zaidi ya saba, nusu, zaidi ya nusu, kati ya nne na tisa* n.k.

Wataalamu wengine huvigawa vitangishi-kuna katika makundi madogo madogo kama vile vitangishi visivyoeleza kiasi au idadi ya vitu vilivyomo katika seti kwa mfano, *fulani*; na vitangishi vinavyoeleza kiasi au idadi ya vitu vilivyomo ndani ya seti kwa mfano *baadhi, kadhaa, chache, -ingi* n.k. (taz. Szabolcsi, 1996). Hata hivyo, kuna mazoea ya kufasili vitangishi vingine vyote kirasmi, isipokuwa vitangishi-ulimwengu, kwa kuvihusisha na kialami cha seti isiyo tupu (yaani *kuna*). Vilevile, waandishi wengine hufasili vitangishi kwa ngazi za uimara. Kwa mfano, vitangishi-ulimwengu huchukuliwa kuwa imara kuliko vitangishi-kuna. Kwa mfano *kila* na *-ote* huchukuliwa kuwa imara kuliko *-ingi* au *baadhi* (taz. Lyons, 2011). Hii ni kwa sababu vitangishi-ulimwengu huhitaji vitu vyote vinavyowakilishwa na fahiwa ya nomino iliyokumbwa na kitangishi kuwamo katika seti. Katika makala haya nitajadili aina mbili tu za kwanza za vitangishi. Kwa ujumla, mjadala juu ya aina mbili za kwanza za vitangishi utatoa mwanga ambao unaweza kusaidia kufasili virai vitangishi vingine. Ikumbukwe kwamba

kila aina ya kitangishi ina namna yake ya kuleta utata pale inapotumika na kiashiria kingine cha kimantiki au pale inapotumika na aina nyingine ya kitangishi. Kanuni ya jumla inayoonekana kufanya kazi kwa karibu aina zote hizi za vitangishi ni kuwa kama kuna kitangishi kimoja tu katika tungo na pia hakuna kiashiria kingine chochote cha kisemantiki kilichotumika katika tungo hiyo, vitangishi hivi huwa havileti utata wa kimawanda katika tungo[2]. Kwa mfano, linganisha mifano yenye kitangishi kimoja katika (2) na ile yenye vitangishi viwili au yenye kitangishi kimoja na/au kiashiria cha kisemantiki kimoja katika (3):

(2)
- a. *Kila mtoto* anakula.
- b. Sofia alimtukana *mwanamume fulani.*
- c. Mariamu alinunua *kitabu.*
- d. Rugatiri anaongea *lugha mbili.*
- e. Sadiki amefua *nguo nyingi.*

(3)
- a. *Kila mtoto* anakula *chungwa.*
- b. *Wazazi wote* walimtukana *mwanamume fulani.*
- c. Hakuna mtoto *aliyenunua kitabu.*
- d. *Kila mwalimu* anaongea *lugha mbili.*
- e. *Watoto wote* wamefua *nguo nyingi.*
- f. *Kila mjamzito* anampenda *daktari gani?*[4]

Kila tungo katika (2) ina kirai kitangishi kimoja tu. Hata hivyo, virai hivi haviwezi kufasiliwa kimawanda kutokana na ukweli kwamba hakuna "vichukua mawanda" vingine katika tungo. Mfano wa 2(a) hauna utata wowote. Katika lugha nyingi kitangishi *kila* kinatajwa kuwa na asili ya utawanyi maana (taz. Mattewson, 1999). Asili hiyo haijamotishwa katika mfano huu kwa kuwa *kila* haijatumika na kitangishi kingine au kipashio kingine cha kimantiki katika tungo. Maana ya jumla inayochanuza hapa ni kuwa kila mtoto katika ulimwengu wa watoto uitwao *y* anakula. Vilevile, hakuna utata katika mifano 2(b)-(e). Sababu yake ni kuwa katika taaluma ya uarifu wa kimantiki majina yote ya pekee hayaingiliani kimawanda na virai vitangishi au viwakilishi vingine vya kimantiki. Hali hiyo inaelezwa pia kwa nomino zinazotambulishwa na vibainishi bayani kama *the* katika Kiingereza (taz. Krifka, 2003) au mofimu kama yambwa katika lugha za Kibantu (ling.

---

[2] Dhana ya mawanda tutaizamia katika sehemu ya 3.3. Kimsingi, kundi hili la maneno halitofautiani kidhana na aina ya maneno yanayojulikana kama viidadi ambayo ni maneno yatoayo taarifa juu ya nomino kwa kuihusisha na dhana kama vile: kiasi, wingi, uchache, kuwepo au kutokuwepo, kuhesabika, kutokuhesabika, upamwe na utawanyi wa kimaana.

[4] Muundo wa sentensi swali wenye kitenzi chenye mofimu yambwa hauleti athari zozote za kimawanda kutokana na matumizi ya mofimu yambwa hiyo. Hili ni sharti la mahusiano ya uhusika katika tungo. Taz. sehemu ya 3.3 kwa mjadala zaidi.

Gambarage, 2012 na marejeleo yake)[3]. Ni muhimu kutanabahisha kuwa utata wa kimawanda tunaouzungumzia hapa siyo sawa na ule wa kileksika tuupatao katika maneno kama *mbuzi, paa* n.k. au utata wa kisarufi uletwao na mofimu moja tu kwa mfano mofimu ya utendea -i- katika *mama alinipigia mpira.*

Mifano yote katika 3(a-f) ina maana ya ziada angalau moja. Ni muhimu kutanabahisha kuwa wasomaji wanaweza kutofautiana katika jinsi ya kupanga maana zinazotokana na utata wa kimawanda. Kwa mfano, maana ya kwanza ya sentensi kwa mtu mmoja inaweza kuwa maana ya pili kwa mwingine. Kigambe cha 3(a) kina maana zifuatazo zitokanazo na matumizi ya vitangishi katika tungo hiyo. Maana ya (i) kila mtoto anakula chungwa lake mwenyewe. Maana ya (ii) ni kuwa kuna chungwa moja ambalo kila mtoto anakula sehemu yake. Tungo ya 3(b) inatupatia maana zaidi ya mbili. Maana ya kwanza ni kuwa kundi la wazazi kwa ujumla/wote kwa pamoja wamemtukana *mwanamume fulani.* Maana ya pili ni kuwa, katika kundi la wazazi {a, b, c, d...n} mwanamume fulani alitukanwa na mzazi *b*, kisha *e*, kisha *j* mpaka mzazi wa mwisho *n*. Inawezekana pia kupata fasili 'kadirifu' kwa maana kuwa unaweza kupata fasili kwamba mtu fulani alitukanwa na mzazi *a* na *f* kwa pamoja kisha akatukanwa na mzazi *k* na kuendelea hadi mzazi/wazazi wa mwisho katika seti ya wazazi. Tungo ya 3(c) ina maana mbili. Mojawapo ni kuwa, katika seti ya vitabu *z* hakuna hata mtoto mmoja aliyenunua kitabu kimojawapo. Maana ya pili ni kwamba *kuna kitabu (fulani)* na kwamba hakuna mtoto aliyekinunua kitabu hicho. Maana ya kwanza inayojichomoza katika mfano wa 3(d) ni kuwa *kila mwalimu* anaongea lugha mbili ambazo zinatofautiana na lugha waongeazo walimu wenzake. Maana ya pili ni kuwa *kuna lugha mbili* (mfano Kiingereza na Kiswahili) ambazo *kila mwalimu* ana umahiri nazo. Katika mfano wa 3(e) kitangishi ulimwengu *wote* kama kilivyotumika hapa, kinalazimisha sentensi hii kufasilika kwanza kama: *Kwa kundi la watoto x kila mtoto alifua lundo lake la nguo.* Maana ya pili inayojitokeza ni kuwa *kuna (lundo la) nguo ambazo watoto wote walishirikiana kufua.* Sentensi ya 3(f) inatofautina na sentensi nyingine zote kwa sababu imekaa katika muundo wa swali. Tungo kama hii ina utata kwa sababu ina kitangishi kiulizi (gani) ambacho ni kiashiria cha kimantiki chenye uwezo wa kuchukua mawanda tofauti na nomino yake. KN *(daktari)* japo haina kitangishi kinachoonekana bado itafasiliwa kwa kuhusishwa na kitangishi *kuna-fiche* kinachojitokeza katika nomino zisizo za pekee (taz. Krifka, 2003; Heim, 2011; Déchaine na Tremlay, 2011 katika lugha ya Kishona; Gambarage 2012 katika Kinata). Jambo la msingi pia hapa ni kuwa fasili ya sentensi swali hutegemeana sana na masharti-ukweli ya sentensi. Hii ni kusema kuwa sentensi swali siyo kigambe kutokana na ukweli kwamba si lazima kinachoelezwa katika sentensi kiwe ndiyo ukweli wa sentensi katika ulimwengu halisi wa mazungumzo. Hivyo, kwa sentensi swali kama 3(f) inafasilika kuwa *kuna* daktari anayependwa na *kila wajawazito* lakini hatujui ni daktari gani.

[3] Hoja ya mofimu yambwa tutaifafanua tutakapokuwa tunaeleza vizuizi vya mawanda katika 3.

Endapo kirai kitangishi kitachukua mawanda-pana tunapata maana mbili: moja ni ile iitwayo 'orodha ya majibu-jozi' (taz. Szabolcsi, 1996; Reinhart 1997; Winter 1997), kwa mfano (Neema na Furaha wanampenda daktari *fulani*, Zelda, Happy na Asha wanampenda daktari *mwingine* n.k. hadi wajawazito wote waishe). Uwezekano mwingine wa fasili ni wa *orodha ya majibu jozi ya mtu mmoja mmoja*, kusema kila mjamzito anatofautiana na mwenziwe katika uchaguzi wa daktari, hivyo kila mjamzito anampenda daktari wake tofauti. Endapo jibu la swali litakuwa ni hakuna daktari anayependwa, masharti ukweli katika sentensi hii yatakuwa 0 au si kweli (taz. Heim and Kratzer, 2010).

## 3.0 Vitangishi-ulimwengu na Vitangishi-kuna katika Kiswahili

Katika sehemu hii utajadili aina, sifa, tabia, na kufasilika kwa vitangishi tajwa katika Kiswahili. Katika kufanya hivyo, nitatumia nadharia ya kisemantiki ya Uarifu wa Kimantiki ya Pierce (1870) iliyoendelezwa na Frege (1895) na baadaye Russell (1905). Nadharia hii ndiyo inayowika hivi sasa katika kueleza mantiki ya vigambe kirasmi (Heim and Kratzer, 2010 na wengine wengi). Kwa kuwa nadharia hii inahusiana sana na tawi la Sintaksia tutaeleza pia Nadharia Finyizi ya Kisintaksia (Chomsky, 1995). Miega hii miwili ni muhimu sana katika kufasili vitangishi kirasmi[5].

## 3.1. Tabia na Vialami vya Kimantiki

### *3.1.1 Vitangishi-ulimwengu*

Vitangishi-ulimwengu (*universal quantifiers*) huandikwa kwa alama ya kimantiki ambayo ni herufi kubwa A iliyopinduliwa juu-chini ($\forall$). Tumetaja awali kuwa kuna vitangishi-ulimwengu vikuu viwili katika Kiswahili ambavyo ni *kila* na *-ote* (taz. Krifka na Zerbian 2008). *Kila* hutumika kukumba nomino iliyo katika umoja (4), na -ote hutumika kukumba nomino iliyo katika wingi, (5).

(4) a. <u>Kila</u> mtoto anakula ndizi.
b. *<u>Kila</u> watoto wanakula ndizi.
c. Kila kundi la watoto linakula ndizi.

(5) a. Watoto <u>wote</u> wanakula ndizi.
b. *Mtoto <u>wote</u> anakula ndizi.

Katika mfano wa 4(b) kitangishi ulimwengu *kila* hakiwezi kutumika kukumba nomino iliyo katika wingi. Mfano wa 4(c) ni sahihi kwa sababu kitangishi kinakumusha nomino *kundi* na kirai kihusishi chake, siyo nomino *watoto*. Mfano

[5] Nadharia Finyizi ni tafsiri ya 'Minimalist Program' ya Chomsky (1995) na baadaye Chomsky (2000, 2001). Ninatumia neno nadharia japo Chomsky mwenyewe anaeleza kuwa hii si nadharia bali ni programu. Wataalamu wengi huitaja kama nadharia kama ninavyofanya hapa.

wa 5(a) uko sahihi lakini siyo 5(b) kwa sababu *wote* haiwezi kukumba nomino iliyo katika umoja. Vitangishi hivi vinashabihiana kisemantiki kutokana na ukweli kwamba vyote vinahusishwa na kufanya kirai-kitangishi kufasilika na 'maana tawanyi'. Tofauti baina ya aina hizi za vitangishi ni kuwa kitangishi *kila*, kinatajwa katika lugha nyingi kuwa 'kiasili' kina nduni [+tawanyi]. Kitangishi -*ote*, kwa upande mwingine, nduni hiyo si sifa yake asilia (ling. Begheli na Stowell, 1996 katika Kiingereza). Kwa maneno mengine ni kuwa, -*ote* mara nyingine, hufasilika na maana-pamwe. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa matumizi ya vitangishi-ulimwengu hutaja kuwa kila kitu kinachohusika na seti ya nomino tajwa kimo katika seti hiyo. Kwa mfano, katika mfano wa 2(a) itakuwa ni ukinzani wa hali ya juu kama utasema kuwa *#kila mtoto alikula ndizi lakini kuna baadhi hawakula.*

*3.1.2 Vitangishi-kuna*

Vitangishi-kuna (*existential quantifiers*) katika nadharia ya Uarifu wa Kimantiki huandikwa kwa herufi kubwa "E" iliyogeuziwa kushoto (∃). Neno "kuna" litatumika hapa kutokana na fahiwa yake kuwa ndiyo sifa ya msingi ya kundi hili la vitangishi. Neno hili linamaanisha kuwa seti ya vitu haiko tupu. Hapa tunajadili vitangishi-kuna ambavyo fahiwa yake inakaribiana na ile ya kitangishi *some* tulichokitolea mfano katika (1). TUKI (2001) wanatoa mwongozo mzuri wa namna ya kufasili neno *some* katika Kiswahili. Fasili yao, ambayo nakubaliana nayo kwa kiasi kikubwa, inadhihirisha kuwa kitangishi hiki kinafasilika kutoka na nomino kinayoikumba[6]. Nitatumia mifano waitowayo TUKI kwa sababu inajitosheleza:

(6) a. Nataka chakula *(kiasi)*.
'I want *some* food'

b. Watoto *baadhi/wengine* hawapendi shule.
'*Some* children don't like school'

c. Anafanya kazi katika ofisi *fulani* mjini.
'He works at *some* office in town'.

d. Walitumia muda *mwingi/kiasi* wakitafuta malazi.
'They spent *some* time looking for accommodation'.

e. Wanafunzi *kama/wapatao* hamsini waliandamana.
'*Some* fifty students demonstrated'.

---

[6] TUKI (2001) wanaona kuwa neno *some* limetumika kama kivumishi (*adjective*) katika mifano ya Kiingereza 6(a-d); kielezi katika 6(e); na limetumika kama kiwakilishi (*pronoun*) katika 6(f).

f. *Baadhi/sehemu ya* marafiki zake hawakubali
'*Some of* his friends do not agree'.

Mifano hii inaonesha wazi kuwa kitangishi *some* cha Kiingereza hakina tafsiri moja katika Kiswahili kama tulivyofikiri kabla. Badala yake kitangishi hiki kinatafsirika kulingana na muktadha wa sentensi ya Kiswahili. Wataalamu kadhaa wanakitaja kitangishi-kuna kuwa ni kijenzi cha sentensi zenye mzio si-kanushi. Hivi kusema huamrishwa kiuambajengo na kiambajengo si-kanushi katika sentensi. Kwa mfano, kitenzi si kanushi katika Kiswahili. Kama ukibadilisha hali ya sentensi katika (6) na kukiweka katika ukanushi utaona kuwa sentensi zote za Kiingereza zitakuwa na utosarufi. Kwa upande mwingine, si sentensi zote za Kiswahili zitakuwa na ubuyi. Tazama mifano hiyo inavyojitokeza katika (7).

(7) a. Sitaki chakula *chochote/#(kiasi).*
'I don't want *any/*some* food'.

b. Hakuna watoto *wowote/#baadhi/#wengine* ambao hawapendi shule.
'There are no *any/*some* children who don't like school'.

c. Hafanyi kazi katika ofisi *yoyote/#fulani* mjini.
'He doesn't work at *any/*some* office in town'.

d. Hawakutumia muda *wowote/mwingi/kiasi* kutafuta malazi.
'They didn't spend *any/*some* time looking for accommodation'.

e. Hakuna wanafunzi *wowote/#kama/#wapatao* (hamsini) walioandamana.
'There are no *#any/*some* fifty students who demonstrated.

f. Hakuna *baadhi ya/sehemu ya* marafiki zake (*wowote)* ambao hawakubali.
'There is no *any of/*some of* his friends who do not agree'.

Tunaweza kuona kuwa vitangishi-kuna vya Kiswahili havikubaliki kutumika katika sentensi kanushi kama ilivyo '*some*' katika Kiingereza, na badala yake kuna matumizi ya kitangishi ulimwengu *'-o-ote'* kinachotafsirika kama *any* ambacho ni kipashio kinachojitokeza katika sentensi zenye mzio kanushi tu. Tunaona kuwa vitangishi-kuna vingi vya Kiswahili (vilivyowekewa alama #) vinahitaji muktadha wa kimatumizi unaoviruhusu kutumika hivyo. Kwa mfano, jaribu kusema 7(c)

hivi: *Siyo kwamba tu hafanyi kazi katika ofisi fulani mjini, ni kwamba hafanyi kazi kabisa/katika ofisi yoyote mjini.* Tunaona pia kwa kutumia kiunzi jaribio cha ukanushi tunapata kuhama kwa maana ya baadhi ya vitangishi. Kwa mfano, *wengine* katika 7(b) itatafsirika kama 'other' zaidi na siyo 'any'. Sentensi itasomeka *hakuna watoto wengine (wowote) waliosalia ambao hawapendi shule;* sentensi inayotafsirika karibu sawa na *'there are no any other children left who don't like school'.* Mfano wa 7(d) vitangishi *mwingi* na *kiasi* vinatumika bila shida katika muktadha wa tungo kanushi isipokuwa vitangishi hivi vimeacha maana yake ya awali na sasa vitatafsirika kama '*a lot*' na *little*' mtawalia. Mfano wa 7(e) unasomeka zaidi kama *hakuna wanafunzi wowote/hamsini walioandamana.* Kwa kuweka pamoja kitangishi na *neno-namba* (number word) kunafanya tungo hiyo kuwa na ukakasi katika lugha zote mbili. Tunahitimisha hoja hii kwa kusema kuwa, muktadha hulazimisha matumizi ya vitangishi-kuna.

Hoja nyingine ya msingi ni kuwa kuna matumizi ya kitangishi-kuna *fiche* katika Kiswahili. Hoja hii inaungwa mkono mahali pake pa kwanza na mfano uliotolewa na TUKI (2001) katika 6(a). Mabano yaliyowekwa katika kitangishi *kiasi* yanaashiria kuwa unaweza kusema tungo hiyo bila neno hilo na bado maana ikawa sawa na ile inayodokezwa na tafsiri ya Kiingereza. Zingatia miktadha ya kitangishi *fulani* katika (8) na (9).

*[Muktadha: Unatembea njiani, unakutana na kijana muuza machugwa ambaye humjui. Unamsifia kwa kusema kuwa machungwa yake (katika kikapu cha wazi kwenye baiskeli) ni makubwa na mazuri. Anakupa chungwa. Unapofika nyumbani mmoja wa wanafamilia ambaye amekuwa akilalamika siku zote kuwa huna hela, anakuuliza, "Nani amekupa chungwa?" unamjibu (8)].*

(8) a. Kijana *fulani* (amenipa).
b. #Kijana (amenipa).

*[Muktadha: Marafiki zako wawili mke na mume (Juma na Maria) wamekuja kukusabahi. Umewapelekea maji ya kuoga maliwatoni na wameamua kwenda kuoga pamoja maliwatoni, ambako pia ndiko msalani. Mpita njia (ambaye hawajui wageni wako) amebanwa na haja ndogo, anapita na kukuambia "Naomba kutumia choo chako mara moja". Kwa kuwa unajua (Juma na Maria) bado wanaoga, unamjibu (9)].*

(9) a. Subiri kidogo. Kuna *watu* wanaoga.
b. (#)Subiri kidogo. Kuna watu *fulani* wanaoga[7].
c. #Subiri kidogo. Watu *fulani* wanaoga.

---

[7] Msemaji wa Kiswahili niliyemhoji juu ya muktadha wa (9), alionekana kukubali mfano wa 9(a) zaidi kuliko 7(b) kwa maelezo kuwa ukisema 7(b) ina maana kuwa hata wewe huwajui watu wanaooga.

d. #Subiri kidogo. Juma na Maria wanaoga.

Kwa muktadha ulioelezwa katika (8), unaposema sentensi 8(b) unamaanisha kuwa msikilizaji wako ana taarifa fulani juu ya kijana huyo. Tunaweza kusema kuwa majibu 9(a) na 9(b) yanakamilishana. Huu ni uthibitisho kuwa msemaji anaweza kutotumia kitangishi *fulani* katika usemaji wake lakini neno hilo bado likawa na matumizi akilini mwake (taz. Chomsky 1995 na kazi zake za baadaye). Waandishi wengi hukubaliana kuwa nomino zote isipokuwa nomino za pekee (yaani zenye sifa za ubayani) na zile zinazotambulishwa na vibainishi, mfano *the* katika Kiingereza, zinafasilika kwa kuhusihwa na kialami ∃. Kwa mfano, katika lugha ya Kiingereza kirai 'a boy' kinachukuliwa kuwa na maana ya 'some boy' hata kama 'kitangishi some' hakikutumika katika kirai cha awali (taz. Krifka, 2003). Hoja hii huhusisha pia nomino ambazo hazijatambulishwa na vibainishi (bare plurals) kwa mfano *'gold was exctracted'* ina maana sawa na *'some gold was exctracted'* (taz. Fodor na Sag, 1982; Krifka, 2003 na wengine). Ushahidi mwingine wa ukapa wa *kitangishi-kuna* ni ule wa kimawanda katika nadharia ya Uarifu wa Kimantiki ambapo nomino zisizo za pekee huchukua mawanda na hufasilika kwa kuhusishwa na kitangishi kuna (au kialami ∃), wakati zile za pekee hazichukui mkabala huu (rejea mifano katika (2) na (3)). Tuhitimishe mjadala wa vitangishi-kuna kwa kusema kuwa vitangishi hivi vikumbapo nomino haviifanyi nomino kudokeza maana kwa mtindo wa "upamwe", "utawanyi", au "kila kitu kinachohusika na nomino tajwa kuwa kimo katika seti" kama ilivyo kwa vitangishi-ulimwengu. Kitangishi-kuna jumui hufanya kirai-kitangishi kufasilika kuwa, idadi ya memba katika seti ya nomino tajwa inaanzia moja na kuendelea, na kamwe siyo ina memba kati ya 0 na $0.9^n$. Kigezo cha uunganishaji kitatusaidia kuonesha jinsi vitangishi-ulimwengu na vitangishi-kuna vinavyotofautiana kisintaksia-semantiki.

(10) a. Watoto *fulani* walizaliwa Kenya na *wengine* (walizaliwa) Tanzania.

b. #Watoto *wote* walizaliwa Kenya na watoto *wengine* (walizaliwa) Tanzania.

(11) a. (Kuna) watoto walizaliwa Kenya na *wengine* walizaliwa Tanzania.

b. #Watoto *wote* walizaliwa Kenya na *wengine* walizaliwa Tanzania.

Mifano katika (10) na (11) inaonesha wazi kuwa unaweza kugawanya seti ya watoto endapo tu nomino katika seti husika imekumbwa na kitangishi-kuna (ling.

10a na 11a) au ni nomino ya kawaida lakini siyo kitangishi-ulimwengu (ling. 10b na 11b). Katika makala haya tutachukua mtazamo wa waandishi kama Kratzer (1998), Krifka (2003), na Déchane na Tremblay (2011) wanaofasili nomino zote zisizo za pekee ambazo hazikukumbwa na kitangishi chochote kwa kuzihusisha na kitangishi-kuna.

*3.1.3 Kikanushi kama Kiashiria cha Kimantiki*

Ukanushi unaelezwa na waandishi wengi kama aina ya kitangishi (kitangishi-kanushi) (taz. Szabolcsi, 1996 na Begheli na Stowell, 1996). Katika nadharia ya Uarifu wa Kimantiki kikanushi huandikwa kwa kialami (¬). Tofauti na vitangishi vingine, kitangishi kanushi kikumbapo nomino huifanya seti hiyo ya nomino kuwa seti tupu. Mfano, kikanushi ni kama vile kitenzi kanushi *hakuna* au mofimu ya ukanushi katika kitenzi cha Kiswahili, (12). Tunakubaliana na Ngonyani (2001) anayeeleza kuwapo kwa kirai-kanushi katika kitenzi kanushi ambacho hutokea juu ya kifundo cha kirai-kitenzi.

(12) a. Mtoto *ha*kula chungwa
b. Hakuna mtoto aliyekula chungwa


Mifano hii inaendana kabisa na ule uliotolewa katika 2(c). Kwa sababu ya matumizi ya kanushi tunapata maana mbili katika kila tungo. Kikanushi kinapochukua mawanda-pana tunapata maana isemayo hakuna mtoto aliyekula chungwa. Endapo kikanushi kitachukua mawanda-finyu, maana itakayochomoza ni ile isemayo kulikuwa na chungwa (fulani) na kwamba hakuna mtoto aliyelila.

**3.2 Mawanda katika Mchoroti na Kanuni Rasmi**

3.2.1 *Mawanda katika Mchoroti: Mwega wa Kinadharia wa I*

Mawanda hupatikana kwa kanuni ya uhamishaji. Chomsky (1995) anatoa hoja kuwa lugha nyingi duniani huruhusu baadhi ya vipashio kuhamishwa bila msemaji wa lugha kuhisi uhamishaji huo. Aina hiyo ya uhamishaji nimeiita *uhamishaji-fiche* yaani unatokea katika akili ya msemaji wa lugha lakini haujioneshi katika muundo wa lugha. Chomsky anatumia kielelezo mfano wa herufi Y iliyopinduliwa juu-chini (13) kuonesha aina mbili za miundo ya sentensi.

(13)



Katika kielelezo hiki cha Chomsky, michakato yote ya kimofofonolojia na kisintaksia kwa mfano, udondoshaji, uongezaji wa vipashio, uhamishaji n.k. hufanyika kati ya muundo-ndani na muundo-nje[8]. Athari za michakato hii hujitokeza wazi katika umbo la kifonetiki la lugha (yaani umbo linalodhihirishwa na kile msemaji asemacho. Umbo hili huitwa "umbo la kifonetiki" (U-Fonetiki) ambalo ni upande wa kulia wa kielelezo. Kwa upande mwingine, michakato inayotokea kati ya muundo nje na muundo ndani huweza pia kutokea kati ya muundo-nje na umbo mantiki (U-mantiki) (kushoto). Michakato hii hutokea katika akili ya msemaji na haijidhihirishi katika umbo la nje la lugha. Hivi ni kusema haitamkwi/haisikiki wala haivumi kwa sababu ni michakato inayohusika na semantiki/mantiki (ling. pia na Carnie, 2007). Ni muhimu kujua japo kwa juujuu tu kwa sasa kuwa, huwa hakuna mawasiliano kati ya U-mantiki na U-fonetiki, isipokuwa kupitia kitengo cha sintaksia.


Baada ya kutoa utangulizi wa juujuu wa muundo wa nadharia finyizi, hebu sasa turejelee suala ambalo tumekuwa tukilijadili. Tumeeleza kuwa utata katika fasili za vitangishi huweza kuzongolewa pale tutumiapo mawanda katika kufasili tungo hizi. Tuchukue mfano wa sentensi ifuatayo:

(14) *Kila mwanamume* anampenda *mwanamke fulani*.


Hapa tayari utakuwa umehisi jambo kuhusu fasili tunazotaka kuziweka bayana kutoka tungo hii. Mchakato mzima wa ujengaji wa sentensi hii, kwa mfano, kuweka pamoja aina za maneno, kuhakikisha kuwa ina upatanisho wa kisarufi unaofaa hadi kufikia kutamkwa, unatokea kati ya M-ndani hadi U-fonetiki. Ni ukweli usiopingika kuwa maana ya kwanza tunayoipata hapa ni ile inayohusu muundo unaoshabihiana na kile kinachosemwa. Msomaji ana uhuru wa kufanya maana ninayopendekeza hapa kuwa ya kwanza, kuwa ya pili kwake endapo hiyo ndiyo fasili inayomjia kwanza. Tusisitize hapa kuwa upangaji wa maana unaweza kutofautiana baina ya mtu mmoja na mwingine. Michoroti katika 15(a) na 15(b) inaeleza maana ya (1) yaani: *Kila mwanamume ana mwanamke wake peke yake anayempenda.*

[8] Dhana ya muundo ndani iliondolewa kabisa katika kazi za baadaye za Chomsky (taz. Chomsky, 2000 na 2001) ambazo pia nafasi ya Muundo-nje imechukuliwa na hatua ya "spell-out" Mabadiliko haya pia yalifanya kielezo katika (13) pia kuchorwa kama Y au T iliyolazwa badala ya kuwa wima.

15(a)




15(b)





Ujengaji wa michoroti ya Kiswahili umetumia kanuni za Nadharia Finyizi isipokuwa kanuni moja tu ambayo sikuona umuhimu wa kuitumia. Kanuni yenyewe ni kuondoa 'kifundo X-ritifaa' (X-bar node). Nadharia Finyizi, pamoja na mambo mengine, inatafuta kurahisisha/kufupisha uwasilishaji wa virai/viambajengo katika mchoroti. Unaweza kuondoa X' katika tungo hizi na mahali pake ukarudia kifundo cha juu yake. Hivyo, ni kusema nimetumia kanuni za 'Nadharia ya Utawala na Ufungamanisho' kwa kukiacha kifundo X-ritifaa. Linganisha pia na mchoroti wa Kiingereza kwa vionjo zaidi vya 'Nadharia ya Utawala na Ufungamanisho'. Nimependekeza tafsiri ya misimbo ya Kiingereza katika 15 (a) kama ifuatavyo: CP ni 'Complimentizer Phrase' ambayo hapa tumeiita Kirai Kijalizo/Jalizi (KJ). IP ni 'Inflectional Phrase' hapa tumeiita ni Kirai Ambatizi (KA) (taz. Gambarage, 2011 kwa dhana ya uambatizi). Kumbuka Kirai ambatizi siyo kiini/shina la kitenzi, japo kifundo cha Kirai Kitenzi hutawaliwa na Kirai Ambatizi. Kwa mujibu wa Barrett-Keach (1980), Krifka (1995) na Ngonyani (1999; 2001) Kirai Ambatizi kinachukua viambishi vya nyakati na vile vya nafsi tu. Nadharia za kileo hubomoa kirai kitenzi ili kupata nafasi ya virai vingine kama tunavyofanya hapa (taz. Rizzi, 1997 kwa virai zaidi). Msimbo AgrOP ni 'Agreement Object Phrase, tuuite 'Kirai Yambwa' ili kuepuka utorojo wa kusema 'Upatanisho wa Yambwa' (KY) (taz. pia Barrett-Keach, 1980); Krifka, 2000). Kirai hiki hubeba kiambishi cha yambwa. Kwa uhakika, unaweza kuchopeka pia kifundo kiitwacho 'Agreement Subject Phrase (AgrSP)' yaani *Kirai Upatanisho wa Mtenda* kati ya KA na A-ritifaa (A') (Inflection bar (I') ambayo haitakuwa na madhara kwa uchambuzi wetu huu wa kinadharia. Misimbo mingine yote inafahamika, kwa mfano QP ni Kirai Kitangishi (Ktan/Kta). NP ni 'Noun Phrase' ambayo ni Kirai Nomino (KN), V ni 'verb' yaani kitenzi na Q ni 'quantifier' yaani kitangishi. Ninaungana na watalaamu wengine lukuki wanaoamini kuwa KN yoyote au hata Kirai-Kitangishi huzalishwa kwanza chini katika uvungu wa KT/Kt na kisha kuhamia juu katika mahali pake inapotamkiwa

(taz. Koopman na Sportiche, 1991; Ngonyani, 1998 katika Kiswahili[9]). Sababu ya kufanya hivi ni kuwa na muundo unaokiweka kiarifu kuwa karibu na vipashio vyake. Kwa ujumla, maana inayoelezwa hapa inatokana na Ktan kuwa juu kabisa katika mti hivyo kuchukua mawanda-pana zaidi ya KN/Ktan iliyo chini yake.

Sasa tugeukie maana ya pili ya kigambe ambayo tutaipata kutokana na Ktan *mwanamke fulani* kuchukua mawanda-pana. Swali ni kuwa tutahamishaje Ktan kutoka kule chini? Tazama mchoroti katika (16).

(16)




Maana inayopatikana baada ya ubadilishanaji mawanda wa virai vitangishi ni kuwa *kuna mwanamke mmoja katika ulimwengu w ambaye kila mwanamume anampenda*. Waandishi wengine (taz. Carnie 2007 katika Kiingereza) wangeiacha Ktan katika uvungu wa KT lakini sisi hatuoni kama hoja hii inamotishwa katika Kiswahili kwa sababu tunapofanya hivyo tunapata U-fonetiki isemayo "**mwanamke fulani ana-m- kila mwanamume penda*", kitu ambacho si Kiswahili. Zingatia pia kuwa kwa kuwa nomino hapa inahusu nomino huifu (binadamu) hatuwezi kuacha kuongeza kipashio yambwa katika kitenzi (taz. Khamisi, 1985). Hii ni kusema kuwa, kila wakati unapokuwa na maana akilini inayoendana na kigambe katika (16) huwa umehamisha kirai tangishi *mwanamke fulani* na kukipa mawanda-pana kuliko kirai *kila mwanamke*; uhamishaji huu hautajionesha katika umbo la nje la kigambe katika (14). Uhamishaji huu unaelezwa kutokea katika akili ya msemaji. Huu ni utaratibu wa kawaida katika ulimwengu wa Nadharia Finyizi.

Halikadhalika, kikanushi kama kiashiria cha kisemantiki hufuata mkabala huu wa fasili ambapo utata unazongolewa kulingana na mawanda ya kirai kitangishi au kikanushi. Tuangalie tungo katika (17) ambayo ina kirai kanushi (Kkan/Kka) na kirai kitangishi ulimwengu.


---

[9] Kuzalishwa kwa mtenda katika uvungu wa KT au Kt si dhana ya leo. Dhana hii ni ya kale tangu kwa Koopman na Sportiche (1991) na imeonesha kufaa katika kutoa maelezo ya uhamaji wa vipashio kama KN, Ktan hata KT katika lugha kama ya Kifaransa, Kiingereza na nyinginezo. Hata hivyo kuna aina mbili za KT: Kirai Kitenzi chenye kitenzi kikuu na Kirai-Kitenzi saidizi (Kt) (*light verb Phrase* (vP)) ambacho hasa kiasilia ndicho kinachotajwa kuwa na uvungu wa atokeapo mtenda.

(17) Watoto *wote ha*wakusoma *kitabu.*


Kama nilivyoeleza katika sehemu ya 1.3.1, nomino zisizo za pekee hufasiliwa kwa kuhusishwa na kirai kitangishi-kuna hata kama kirai hicho hakijioneshi katika tungo. Utungo huu unatupatia maana ya kwanza ambayo ni: Watoto wote hawakusoma vitabu vyao (kila mtoto na kitabu chake). Maana hii ni telezi kutokana na ukweli kwamba kitangishi *wote* huwa hakifanyi vizuri wakati mwingine katika kuleta maana tawanyi. Fasili hii inatujia baada ya kirai tangishi ulimwengu kuwa na mawanda-pana dhidi ya kitabu pia dhidi ya kiashiria kanushi cha kimantiki. Maana hii inaweza kuelezwa na mchoroti katika (18) ambao unafanana na ule wa Ngonyani (2001: 30) katika Kiswahili.

(18)




Maana ya pili ya tungo hii inapatikana kwa kuipa nomino kitabu mawanda-pana kama inavyooneshwa katika (19) (taz. Demuth na Harford (1999) katika Kiswahili na lugha nyingine.

(19)




Katika (19) haiwezekani kuiacha nomino na kitangishi chake katika uvungu wa Kirai Ambatizi kwa sababu mofimu kanushi haiwezi kuingia kati ya nomino ya juu katika mti na kirai tangishi hicho. Kigambe hiki sasa chaweza kufasilika kuwa

kuna kitabu fulani ambacho watoto wote hawakusoma. Baada ya kuona jinsi tunavyoweza kufasili sentensi mbalimbali zenye virai-tangishi hebu tuangalie suala la uandishi wa kanuni za kirasmi zinazoendana na fasili tulizotoa hapa.

3.2.2 *Mawanda katika kanuni rasmi: Mwega wa Kinadharia wa II*

Katika nadharia ya Uarifu wa Kimantiki, vitangishi vilivyojadiliwa hapa pamoja na viashiria vingine vya kisemantiki vinaweza kuandikwa kwa vialami tulivyovitaja mwanzoni. Jambo la msingi hapa linahusu kaida za uandishi ambazo ni rasmi. Uandishi wa kanuni unarejelea mahusiano kati ya kiarifu na vijalizo vyake (ling. na Heim and Kratzer, 2010). Mathalani, chukua kitenzi *cheza* katika tungo kama *Mwanahawa anacheza ngoma* kinachukuliwa kuwa na nafasi mbili kwa kila nomino, yaani nafasi moja kwa {ngoma} na nyingine kwa {Mwanahawa}. Hali kadhalika, vitangishi vinachukuliwa kuwa ni viarifu ambavyo hubeba *vitoshelezi*, ambavyo hapa ni nomino. Jambo la msingi hapa ni kuwa vitoshelezi vya kiarifu huwa vinaandikwa kwa herufi kwa mfano x, y, z, n.k. Vitoshelezi si vitu halisi bali ni vibeba nafasi za vitu halisi katika ulimwengu halisi[10]. Virai vifuatavyo vinaoneshwa jinsi vinavyoandikwa kikanuni katika nadharia hii:

| | | |
|---|---|---|
| (20) | a. | Kila mtu alicheza |
| | b. | $\forall x$[alicheza(x)] |
| (21) | a. | Mtu fulani alicheza |
| | b. | $\exists x$[alicheza(x)] |
| (22) | a. | Hakuna mtu alicheza |
| | b. | $\neg\forall x$[alicheza(x)], au |
| | c. | $\exists x$ $\neg$[alicheza(x)] |

Katika kanuni zilizoandikwa katika (20-22) kila kanuni inaeleza kitu katika ulimwengu halisi kinachowakilishwa na herufi x. Hivyo, 20b inasomeka: kwa vyote viitwavyo x, x alicheza. Kanuni ya (21) tunasoma: Kuna x katika ulimwengu halisi na x alicheza. Mfano wa 22(a) unaandikwa katika 22(b) kuwa hakuna ulimwengu wa vitu viitwavyo x, kiasi kwamba x alicheza. Pia, unaweza kuandikwa kama 22(c), kuna vitu viitwavyo x, lakini hakuna x aliyecheza. Kwa ufupi utaona kuwa vitangishi/viashiria vya kisemantiki vimewakilishwa na vialami vya kimantiki na vitu, mfano *mtu*, vimewakilishwa na herufi. Kwa ufupi utaona

---

[10] Kutokana na mahitaji ya kuweka bayana kirai *katika ulimwengu halisi wa kigambe'* baadhi ya watalaamu wa semantiki hutumia alama (mfano, $\lambda$P) kumaanisha masharti ukweli ya kigambe. P ni kigambe. Hatutafuata mkondo huu wa uandishi wa alama katika makala haya.

hapa kuwa kitangishi/kiashiria cha kimantiki kinachukua mawanda dhidi ya *kitoshelezi* chake. Hii ni sababu ya kinadharia inayokipa nafasi kitangishi/au kiashiria cha kimantiki kuwa mkuu wa kirai. Hapa kitangishi ni kiarifu, sawasawa kabisa na kitenzi na nomino zake. Tatizo la kanuni katika (20-22) hata hivyo ni kwamba ni za jumla mno-hazihitaji vitu viitwavyo x wakati vitu hivyo vimebainishwa katika sentensi. Kuondoa tatizo hili kanuni katika (20-22) zinaweza kuandikwa hivi:

(23) a. Kila mtu alicheza = $\forall x[Mtu(x) \rightarrow alicheza(x)]$

b. Mtu fulani alicheza = $\exists x[Mtu(x) \& alicheza(x)]$

c. Hakuna mtu alicheza = $\neg\forall x[Mtu(x) \rightarrow alicheza\ (x)]$, au $\exists x[Mtu(x) \& \neg\ alicheza\ (x)]$

Kwa kuziandika hivyo, tumedhibiti kule kuruhusu kila kitu chenye uwezo wa kucheza kuwa miongoni mwa vitoshelezi vya viarifu. 23(a) inatuambia kuwa kwa vitu vyote viitwavyo x, kama x ni mtu basi x alicheza. Kishale kinamaanisha masharti kuwa "...basi... au ...kisha...". 23(b) inatuarifu: kuna vitu viitwavyo x katika ulimwengu halisi, na kwamba x ni mtu na x alicheza. 23(c) inasema hakuna ulimwengu wa vitu vinavyoitwa x, kiasi kwamba x awe ni mtu na kwamba awe alicheza. Kanuni ya mwisho inasema, kuna vitu vinavyoitwa x, lakini hakuna x ambaye ni mtu na ambaye alicheza. Msomaji atajiuliza vipi kama tungo *Kila mtu alicheza* ingeandikwa kama $\forall x[Mtu\ (x)\ \&\ alicheza\ (x)]$. Jibu ni hapana! Kwa sababu unachosema hapa ni kuwa katika *ulimwengu halisi kila kitu kiitwacho x ni mtu na kilicheza.* Sasa tutakazia kanuni zetu zaidi ili kuwakilisha masharti ukweli ya kigambe ipasavyo. Soma sentensi ifuatayo inayoundwa na kirai-kanushi na nomino isiyo ya pekee/ nomino yenye kitangishi kuna-fiche.

(24) Maria *ha*kununua *kitabu*

Ili kuepuka kutoa maana za vigambe hivi kidhahania tu, tujaribu kuviweka katika miktadha maalumu. Miktadha ninayotumia hapa ilitumiwa katika kazi za wataalamu kama vile Matthewson (1998, 1999), Krifka (2003), Déchaine na Tremblay (2011), Lyons (2011); na Gambarage (mtamboni) kati ya wengine wengi.

*[Muktadha: Wanafunzi wamekwenda kwenye duka la vitabu la Mangi. Mwalimu aliwaambia yeyote mwenye hela anaweza kujinunulia kitabu apendacho. Maria hakuwa na fedha. Wanafunzi wamerudi, sasa wako darasani. Mmoja wao anasema (25)]*

(25) Maria *ha*kununua kitabu

Ili kupata maana sahihi ya sentensi katika muktadha huu, kirai kanushi lazima kipewe mawanda-pana dhidi ya kiashiria cha kisemantiki ambacho ni nomino kitabu. Kwa kanuni rasmi, masharti ukweli ya sentensi hiyo yanaandikwa kama (26).

(26) $\neg$ [∃x [kitabu (x) & [alinunua (x) (Maria)]]

Kanuni katika (26) inasema hakuna x kiasi kwamba x ni kitabu na kwamba Maria alinunua x. Utagundua uandishi wa kanuni katika nadharia ya Uarifu wa Kimantiki unazingatia kuwa yambwa (kitabu, x) iko karibu na kiarifu kuliko mtenda (Maria). Hapa kikanushi kina mawanda-pana.

*[Muktadha: Mwalimu amewapeleka wanafunzi kwenye duka la vitabu la Mangi ili wanunue kitabu cha Kiswahili cha Kufikirika cha Shaaban Robert. Maria alidondosha fedha njiani hivyo hakununua kitabu. Wakiwa darasani mmoja wa wanafunzi anasema (27)]*

(27) Maria *ha*kununua kitabu

Ni bayana kuwa kuna kitabu maalumU ambacho Maria amekosa kununua hapa. Ili kueleza maana ya kigambe inayosemwa katika muktadha huu inabidi kikanushi kichukue mawanda-finyu kuliko nomino *kitabu*, (28).

(28) ∃x [kitabu (x) & $\neg$ [nunua (x) (Maria)]]

Kanuni katika (28) inasema hakuna x kiasi kwamba x ni kitabu na kwamba Maria alinunua x.

Mbinu hii ya kuzongoa utata kwa kutumia kanuni rasmi imefaulu pia katika kuzongoa utata katika tungo zenye vitangishi-ulimwengu. Tuthibitishe dai hili kwa sentensi iliyotolewa kama mfano katika (14) juu ambayo imerudiwa katika (29) kuepuka usumbufu.

(29) *Kila mwanamume anampenda mwanamke fulani.*

*[Muktadha: Kundi la wanaume limekaa kijiweni linacheza bao. Kila mwanamume anataja mpenzi wake tofauti na mwingine na kueleza sifa za mpenzi wake na kwamba kwa nini anampenda mwanamke huyo. Mwishoni muuza kahawa mmoja baada ya kuwasikia wote anasema (30)].*

(30) *Kila mwanamume anampenda mwanamke fulani.*

Kwa muktadha huu, ni wazi kuwa kirai-kitangishi *kila mwanamume* kinachukua mawanda-pana ili kuruhusu sentensi ya (30) kuoana na kanuni katika (31).

(31) $\forall$x [mwanamume (x) $\rightarrow$ $\exists$y [mwanamke (y) & anampenda (y)(x)]][11]

Kanuni katika (31) inafasilika kuwa katika ulimwengu halisi, kwa wote waitwao x, endapo x ni mwanamume, kisha kuna y na y ni mwanamke, kila mwanamume anampenda mwanamke. Hivi ni kusema kila mwanamume ana mwanamke wake anayempenda, na hivyo kiulimwengu kimechukua mawanda-pana. Ni muhimu kufunga kanuni yako kwa kusema katika ulimwengu halisi wa kigambe. Sasa chukulia sentensi hiyo hiyo inasemwa katika muktadha tofauti.

*[Muktadha: Watu wamekusanyika kuwatazama wanamume watatu walevi wanaogombana. Kisa cha ugomvi wao ni kuwa katika mazungumzo yao wamejikuta wote kumbe wana mahusiano na mwanamke mmoja. Kila mwanamume anatoa sababu na kuvutia kwake kwamba yeye ndiye anapendwa na huyo mwanamke kuliko wengine wote. Kijana mmoja anaulizwa na mpita njia kuwa ugomvi ni wa nini. Anasema (29) iliyorudiwa katika (32)].*

(32) *Kila mwanamume anampenda mwanamke fulani.*

Msemaji wa kigambe (32) katika muktadha kama huu ana maana kuwa kuna mwanamke fulani asiyemjua na kuwa mwanamke huyo anapendwa na kila mwanamume. Kigambe hiki kinaweza kuandikwa kwa kanuni ifuatayo katika (33).

(33) $\exists$x [mwanamke (x) & $\forall$y [mwanamume (y) $\rightarrow$ y anampenda x]]

Kanuni katika (33) inasema kuwa kuna mwanamke katika ulimwengu halisi ambaye kila mwanamume anampenda mwanamke huyo. Hapa, kirai *mwanamke fulani* kimechukua mawanda-pana dhidi ya kirai *kila mwanamke*. Nilipomhoji msemaji mwingine wa Kiswahili aliniambia kuwa angependelea zaidi kutumia tungo *wanamume wote wanampenda mwanamke fulani* kuliko kusema (32). Hii ni kutokana na uwezekano kwamba kwa watumiaji wengine *wote* haina nguvu ya utawanyimaana kama ilivyo *kila*. Matthewson (1998; 1999) anaripoti pia kuwa

---

[11] Kuna mifumo mingi ya uandishi kanuni ambayo yote huelekea katika fasili ya aina moja. Kwa mfano, (27) inaweza kuandikwa $\forall$x[mwanamume (x) $\rightarrow$ $\exists$y [mwanamke (y) & x anampenda y]]. Katika aina hii ya uandishi kanuni sehemu ya mwisho ya kanuni inayotaja x na y, haikuzingatia kukiweka kiarifu karibu na nomino. Waandishi wengine hata hivyo hawazingatii upangaji huu wa vijalizo (taz. Ailloud, 2007).

katika lugha ya St'at'imcets, (izungumzwayo Magharibi mwa Canada), kitangishi sawa na *wote* katika katika hiyo kina maana kusanyi wakati wote. Pendekezo la msemaji niliyemhoji linatufungia sehemu hii kwa kusema kuwa katika Kiswahili *kila mwanamume* na *wanaume wote* huweza kutofautiana katika kupanga maana. Vikitumiwa katika tungo tofauti, maana ya kwanza ya tungo tutakayoipata pale kirai kitangishi *x wote* kikiwa na mawanda-pana inaweza kuwa ni maana ya pili kwa tungo yenye kirai kitangishi *kila x* (yenye mawanda-finyu). Vitangishi *kila* na –ote katika Uarifu wa Kimantiki hutabiriwa na kanuni ya aina moja.

### 3.3 Vizuizi katika Mawanda

Katika lugha nyingi duniani, matumizi ya vipashio vya kisintaksia au vya kimofolojia huzuia uzongaji wa utata katika tungo (taz. Lyons, 2011; Gambarage 2012). Dhana hii inathibitika kuwa kweli katika Kiswahili. Vipashio vinavyozuia mawanda huwa kimsingi vina nguvu ya kuzuia mawanda ya upande mmoja na hivyo kuondoa/ kuzuia utata katika tungo. Msemaji anapotumia vipashio hivi huwa anachukulia kuwa msemaji ana maarifa fulani au hana maarifa fulani juu ya kitu kinachorejelewa na (kirai) nomino au kirai kitangishi katika ulimwengu halisi. Tuangalie mifano michache kati ya mingi inayopatikana katika Kiswahili.

Kwanza, tuanze na *kiambajengo cha mzio wa ukanushi*. Mifano katika (5) juu ilituonesha kuwa utiapo ukanushi katika kitenzi, kipashio cha mzio wa ukanushi kinachoamrishwa na kitenzi kanushi ni *–o-ote*. Hivyo, tunapotumia kiambajengo hiki hatutegemei kupata utata katika tungo ya Kiswahili, (34).

(34) Maria *ha*kununua kitabu *chochote*.

Msomaji atakubaliana na mimi kuwa unaweza kusema tungo hii katika muktadha kama uliojadiliwa katika (25) ambapo wanafunzi wangeweza kununua kitabu chochote; lakini siyo muktadha katika (27), yaani walitakiwa kununua kitabu fulani. Ni muhimu kuona pia kuwa inawezekana kusema tungo hii katika mazingira ambayo wanafunzi walipewa uhuru wa kununua kitabu fulani au/na kitabu kingine chochote, kisha Maria hakununua hata kimojawapo.

Pili, *uolezi, urejeshi, na vipashio milikizi* huondoa utata katika tungo. Lugha ambazo hazina vibainishi kama *a* na *the* kama Kiingereza hutumia zaidi vipashio hivi, na baadhi ya vipashio vya kimofolojia katika kuibainisha nomino. Hii ni kwa sababu chanzo cha utata usio wa kileksika ni utobayana (ling. Fodor na Sag, 1982). Tutakubaliana kuwa tungo katika (35) zingekuwa tata kama nomino husika zisingekumushwa na vipashio hivi.

(35) a. Kila mwanamume anampenda mwanamke *huyu*.
b. Kila mwanamume anampenda mwanamke *aliyepewa zawadi na Rais Kikwete*.
c. Kila mwanamume anampenda binti *yangu*.

Ukiondoa maneno yaliyowekwa katika *mlazo* utagundua kuwa tungo hizo zinarudia utata tulioujadili katika sehemu zilizotangulia. Huu ni uthibitisho kuwa matumizi ya neno kisonde (uolezi) (rej. 35a), urejeshi (rej. 35b) na umilikizi (35c) huua utata katika tungo. Tungo zote hizi msikilizaji kupata ubayani wa nomino mojawapo na hivyo nomino hiyo kuondokana na utata. Kwa mfano, wasikilizaji waweza kukosa uelewa kuhusu wanaume wanaosemwa hapa, lakini si mwanamke katika mjadala. Sentensi zote hizi zina umaanilizi tofauti kuhusu mwanamke. Kwa mfano, 35(a) inamaaniliza kuwa mwanamke katika muktadha wa mazungumzo anapendwa, na 35(c) inamaanisha kuwa msemaji anaye binti. Vimilikizi vingine vinavyozongoa utata ni kama vile: *peke yake*, *-enyewe*, n.k.

Suala la ubayani wa maana linatufikisha kwenye kipengele cha mwisho cha makala haya. Hapa tuzungumzie *kipashio yambwa*[12]. Yambwa husemekana pia kuzuia utata unaotokana na matumizi ya vitangishi katika sentensi. Waandishi wengine katika lugha za Kibantu mfano Bresnan and Mchombo (1987) katika Kichewa, Visser (2008) katika Kizulu, Déchaine na Tremblay (2011) katika Kishona, na Gambarage (2012) katika Kinata wanadai kuwa kipashio yambwa, katika lugha hizi, kina kazi maalumu ya kutangaza kuwa msikilizaji ana maarifa ya awali kuhusu kitu kirejelewacho na yambwa hiyo[13]. Katika Kiswahili mtazamo unaokubalika zaidi ni ule wa Berret-Keach (1980), pia Khamisi (1985) kama ulivyoshadidiwa na Krifka (1995) kuwa matumizi ya mofimu yambwa katika Kiswahili yanaelekea zaidi katika matabaka ya uhai kuliko maarifa ya awali ya msikilizaji juu ya kinachosemwa. Berret-Keach (1980) anaeleza kuwa endapo mhusika ni binadamu, lazima yambwa itumike, sharti ambalo halihusu wahusika wasio binadamu. Zingatia sentensi hizi za mwisho katika (36).

| | | | |
|---|---|---|---|
| (36) | a. | (i) | *Kila kijana alipa/alipatia mtoto fulani chakula. |
| | | (ii) | Kila kijana alimpa/alimpatia mtoto fulani chakula. |
| | b. | (i) | *Wazazi wote walisukuma Juma. |
| | | (ii) | Wazazi wote walimsukuma Juma. |
| | c. | (i) | ?Kila mtoto alitukana mzazi[14]. |

[12] Mwandishi hajadili katika makala haya dhana zinazohusika na yambiwa, n.k. kwa sababu mada hizo zinahitaji makala ya peke yake.

[13] Bresnan na Mchombo (1987) wanaichukua hoja ya kipashio yambwa katika hatua nyingine wanapodai kuwa yambwa siyo mofimu inayowakilisha mtendwa/kitendwa bali ni "kiwakilishi halisi" kilichofichama katika kitenzi (incorporated pronoun). Hoja ya mofimu yambwa kuwa kiwakilishi ndani ya kitenzi katika lugha za Kibantu inatolewa mashaka na waandishi kama Krifka (1995) na Ngonyani (2001) katika Kiswahili. Hoja hii si muhimu hapa.

[14] Mhariri wa makala haya alipendekeza kuwa sentensi kama vile 36(c) haziko sahihi sana, tazama pia *2(b) "Sofia alitukana mwanamume fulani" ambayo nimeiongeza mofimu yambwa* baada ya maoni yake. Ni wazi kuwa kuna ngazi za ulazima katika matumizi ya mofimu yambwa ambayo hutegemea mambo kama vile: aina ya kitenzi, aina ya mhusika, aina ya jina (jina la pekee au la kawaida hususan kwa mhusika binadamu), muundo wa sentensi. Kwa mfano, sentensi kama 36(c) inaweza kuwa si sahihi sana kwa sababu ya matumizi ya kitangishi, la sivyo majina ya kawaida yatajayo binadamu yanahitaji muktadha wa kimatumizi ili kuruhusu yambwa isitumike. Swali hili halitajadiliwa kirefu katika makala haya.

(ii) Kila mtoto ali**m**tukana mzazi (#lakini sijui ni mzazi yupi).

d. (i) Kila mtu aliua mnyama (lakini sijui ni mnyama gani)
(ii) Kila mtu ali**mu**ua mnyama (#lakini sijui ni mnyama gani).

e. (i) Wanafunzi wote walinunua kitabu (lakini sijui ni kitabu kipi)
(ii) Wanafunzi wote wali**ki**nunua kitabu (#lakini sijui ni kitabu gani).

Mifano hii ilitaka kuthibitisha endapo kuna ukweli kuwa uongezaji wa yambwa katika kitenzi hudokeza kuwa msemaji ana maarifa fulani juu ya kile kinachorejelewa na mofimu yambwa hiyo. Kama hili ni kweli basi tutatabiri kuwa matumizi ya yambwa yatazuia utata wa kimawanda. Jambo hili linaonekana kuwa kweli kwa upande mmoja lakini si kweli kwa upande mwingine. Kwanza, vitenzi vya shina lenye silabi moja 36(a) havikubali kuacha yambwa kama yambwa ni binadamu. Hapa yambwa haivurugi utata wa tungo. Mfano katika 36(b) hauhusiki na utata kwa sababu nomino iliyotumika ni ya pekee. Hata hivyo, mfano huu pia unatuonesha kuwa matumizi ya nomino ya pekee yanashurutisha matumizi ya mofimu hii katika kitenzi. Mifano katika 36(c), (d) na (e) inaonesha makundi matatu tofauti ya wahusika, yaani binadamu kwa majina pekee, wanyama, na vitu visivyo na uhai, mtawalia. Makundi yote yanaonesha kuwa ni sawa kuacha mofimu hii, na wakati tunafanya hivyo utata tulioujadili hapo juu unachomoza katika tungo hii. Mifano yote yenye alama # inaonesha ukakasi. Ukakasi unajitokeza pale mzungumzaji anaposema ana maarifa juu ya yambwa kisha anarudi kufuta dhanilizo lake kuwa hajui (taz. Lyons 2011; Gambarage (mtamboni)). Hivi ni miongoni mwa vigezo vinavyotuthibitishia kuwa yambwa katika makundi haya ya mwisho ina nguvu ya kuzuia utata wa kimawanda. Ukitafakari kwa makini sentensi *kila mtoto ali**m**tukana mzazi, kila mtu ali**mu**ua mnyama, wanafunzi wote wali**ki**nunua kitabu* utagundua kuwa katika tungo hizi hatuwezi, kwa sababu ya matumizi ya yambwa katika kitenzi, kupata maana tawanyi, kwa mfano, kila mwanafunzi kuwa alinunua kitabu tofauti (36c). Kama maelezo haya ya uhusiano wa yambwa na mawanda yanakinzana na ufahamu wa wanalugha wengine, suala la mofimu yambwa nitaliacha uwanjani kuwa swali la wazi.

### 4.0 Hitimisho

Katika makala haya tumejadili vitangishi vichache tu kati ya vingi katika Kiswahili. Nimeonesha kuwa matumizi ya vitangishi na vipashio vingine ambavyo kiasili ni viashiria vya kisemantiki huleta utata katika tungo. Nimejadili jinsi mbinu ya kupishanisha mawanda inavyosaidia katika kuzongoa utata wa tungo hizi. Pia, nimeonesha kwa kutumia nadharia rasmi, yaani Nadharia Finyizi

(Sintaksia) na Nadharia ya Uarifu wa Kimantiki (Semantiki), jinsi inavyofasili utata huu. Vilevile, nimeonesha kuwa vipashio vya kisintaksia na vya kimofolojia vinavyoweza kutumika kuzuia utata unaotokana na vitangishi. Hali kadhalika, nimeonesha kuwa tungo isemwayo katika muktadha fulani wa mazungumzo haiwezi kuwatatiza watumiaji wa lugha. Sababu yake ni kuwa wasikilizaji huhusisha kigambe na ulimwengu halisi wakati wa mazungumzo. Katika mazingira kama haya wasikilizaji hawawezi kukabiliwa na utobayani wa maana. Tunahitimisha kuwa, wakati aina ya utata tulioujadili hapa huibushwa na kinywa cha msemaji (pengine) bila kujijua, mzigo wa kutafuta masharti ukweli ya kigambe humwangukia msikilizaji. Makala haya pia yameonesha kuwa mada ya vitangishi na mawanda haiwezi kujadiliwa bila kuhusisha vitengo vya lugha kama sintaksia, semantiki, na muktadha wa matumizi (pragmatiki).

## Marejeleo


Ailloud, E. (2007). "Glue Semantics and Dominance Constrints". MA Thesis. M.Sc.Language Science and Technology. Universität des Saarlandes.

Barrett-Keach, C. (1980). The Syntax and Interpretation of the Relative Clause Construction in Kiswahili. Amherst: University of Massachusetts. PhD. Dissertation.

Begheli, F. na Tim, S. (1996). Distributivity and Negation. Katika Anna Szabolcsi (Ed.) *Ways of Scope Taking*. Boston: Kluwer.

Bresnan, J. na Mchombo, S.A. (1987). Topic, Pronoun and Agreement in Chichewa. Linguistics Society of America. Vol. 63, No. 4. 741-782.

Carnie, A. (2007). Syntax: *A Generative Introduction*. 2rd Edition. Oxford: Blackwell Publishing.

Chomsky, N. (1995). "The Minimalist Program". Cambridge, Mass. MIT Press.

______. (2000). Minimalist inquiries: The framework. Katika Step by step: Essays in honor of Howard Lasnik, Wahariri. R. Martin (et al), 89-155. Cambridge: MIT Press.

______. (2001). Derivation by phase. Katika Kan Hale: A life in language, Imehaririwa na M. Kenstowicz, Cambridge, MIT Press. 1-52.

Déchaine, R. na M. Tremblay. (2011). Deriving nominal reference. Paper presented at WECOL 2011, SFU.

Demuth, K. na C. Harford. (1999). Verb Raising and Subject Inversion in Bantu Relatives. Journal of African Languages and Linguistics 20,1: 41-61.

Fodor, J.D I.A Sag (1982). "Referential and Quantificational indefinites". Linguistics and Philosophy 5, 355–398.

Frege, G. (1997 [1892]). On Sense and Reference. Katika P. Ludlow (Mhariri), Readings in the Philosophy of Language, 563–583. MIT Press.

Gambarage, J.J. (2011). "Mkanganyiko wa Dhana za Shina, Kiini, na Mzizi katika Mofolojia ya Kiswahili". *Kiswahili* Vol. 74(1). 12-24.

______. (2012). The Pre-Prefix in Nata: An Interface Account. Itatokea katika Proceedings of the 43rd Annual Conference on African Linguistics.

______. (mitamboni). "Context of Use of Augmented and Unaugmented Nouns in Nata". Itatokea katika UBC Working Papers in Linguistics.

Heim, I. na A. Kratzer (2010). Semantics in Generative Grammar. Blackwell Publishing. University of Massachusetts at Amhert.

Khamisi, A. M. (1985). Kiswahili Verb Derivation. University of Hawaii PhD. Dissertation.

Koopman, H. and Sportiche, D. (1991). The Position of Subject. Lingua 85, 211-258.

Krifka, M. (1995). Kiswahili. Katika J. Jacobs et al. (eds.), Syntax: An International. Handbook of Contemporary Research, Walter de Gruyter, Berlin, 1397-1418.

Krifka, M. and Zerbian, S. (2008). "Quantification Across Bantu Languages". Center for General Linguistics, Berlin.

Lyon, J (2011). The syntax of Okanagan determiner phrases. Katika Papers for the 46th Annual International Conference on Salish and Neighboring Languages , 11-81.

Matthewson, L. (1998). Determiner Systems and Quantificational Strategies: Evidence from Salish, Holland Academic Graphics, The Hague.

______.(1999). On the interpretation of wide scope indefinites. Natural Language Semantics 7, 79–134.

Ngonyani, D. (1998). V –to-I movement in Kiswahili. *Afrikanistische Arbeitspapiere* Juz. 55: 129-144.

______. (1999). $X^0$-movement in Kiswahili Relative Clause Verbs', Linguistic Analysis 29, 137-159.

______. (2001). Evidence for Head Raising in Kiswahili Relative Clauses. Studies in African Linguistics. Volume 30, Numbers 1, 2001.

Pierce C.S. (1870) "Description of a notation for the logic of relatives, resulting from an amplification of the conceptions of Boole's calculus". In Memoirs of the American Academy, 9: 317–78; Imechapishwa tena katika CP, 3.45–3.148.

Pesetsky, D. (Mh.) (2011). Case the Oxford Handbook of Linguistic Minimalism. C. Boeckx.

Pollock, J. (1989). Verbs Movement, Universal Grammar, and the Structure of 18. Linguistic Inquiry 20. 365-424.

Reinhart, T. (1997), 'Quantifier Scope: How Labor is Divided between QR and ChoiceFunctions,' Linguistics and Philosophy 20, 335–397.

Szabolcsi, A. (Mh.) (1996). *Ways of Scope Taking*. Dordrecht. Kluwer.

Russell, B. (1998 [1905]). On denoting. Katika G. Ostertag (Mhariri), Definite Descriptions: A Reader, Cambridge, MA, 35–49. MIT Press.

TUKI (2001). *Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza.* Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Visser, M. (2008) Definiteness and specificity in the isiXhosa determiner Phrase. South African Journal of African Languages. Juz. 1. 11-29.

Winter, Y. (1997). 'Choice Functions and the Scopal Semantics of Indefinites', Linguistics and Philosophy 20, 399–467.

**Orodha ya Istilahi**

| **Istilahi ya makala** | **Istilahi nyingine** | **Kiingereza** |
|---|---|---|
| Dhanilizo | - | presupposition |
| Fahiwa | fahiwati | sense |
| Jozi kadirifu | - | dradable pair/ |
| Kaida | - | etiquette |
| Kiashiria cha kimantiki | - | logic operator |
| Kiasilia | - | inherently |
| Kiarifu | kitenzi | predicate |
| Kigambe | - | proposition |
| Kitangishi | kiidadi | quantifier |
| Kitangishi jumui | - | generalized quantifier |
| Kitangishi kuna | vivumishi vya –ote | existential quantifier |
| Kitangishi ulimwengu | kivumishi cha idadi | universal quantifier |
| Kikumushi | - | modifier |
| Kitenzi kisaidizi | - | aux/light verb |
| Kipashio/ mofimu yambwa | mofimu ya utendwa | object marker |
| Kumba | - | quantify over |
| Maana pamwe | - | collective reading |
| Maana tawanyi | - | distributive reading |
| Maana ya kwanza | - | salient/first reading |
| Maana ya pili | - | second reading |
| Maana ya kigambe | - | propositional meaning |
| Masharti ukweli | masharti ya ukweli | truth conditions |
| Matabaka ya uhai | - | animacy levels |
| Mawanda | - | scope |
| Mawanda finyu, kati, pana | - | narrow, intermediate, wide scope |
| Mzio kanushi | - | negative polarity |
| Mzio si-kanushi | - | positive polarity |
| Nadharia Finyizi | - | minimalist program/theory |
| Nadharia rasmi | - | formal theories |
| Nadharia ya Utawala na Ufungamanisho | - | government and binding (gb) |
| Nduni | - | feature |
| Nomino huifu | - | animate noun |
| Mhusika huifu | - | animate participant |
| Mhusika si huifu | - | inanimate participant |

| | | |
|---|---|---|
| Muktadha | - | context |
| Orodha ya majibu-mozi | - | pair-list answers |
| Thamani ukweli | - | truth value |
| Uarifu wa Kimantiki | - | predicate logic |
| Uambatizi | uambishaji wa kisarufi | inflection |
| Mahusiano ya uamrishi wa kiuambajengo | - | c-commanding relation |
| Ubuyi | uvulivuli | opacity |
| Uelewa | - | familiarity |
| Uhai | uhayawani | animacy |
| Uhamishaji | - | move(ment) |
| Uhamishaji fiche | - | covert movement |
| Uhamishaji wazi | - | overt movement |
| Uhusika | - | partcipants |
| Ukakasi | - | infelicitous |
| Ukinzani | - | contradiction |
| Upelekaji mbele wa vitangishi | - | quantifier raising |
| Uolezi | neno kisonde, kivumishi kioneshi | deixis |
| Umbo-nje la lugha | - | |
| Umbo-ndani la lugha | - | |
| Uvungu | - | specifier |
| Yambwa | mtendwa | object noun |
| Vimaanilizi | - | conversational implicatures |
| Vitoshelezi | - | variables |
| X' (X-ritifaa) | - | x-bar |